

MABADILIKO YA TABIANCHI

Ujenzi wa bandari, viwanda kuathiri mazingira Bagamoyo

Bandari itakuwa na meli nyingi zinazoweza kusababisha uchafu wa mazingira kutokana na matumizi ya mafuta


Julie Ngarabali, Mwananchi

Bagamoyo. Serikali imetakiwa ianze kujipanga kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kabla ya kukamilika kwa ujenzi wa bandari mpya wilayani hapa Mkoa wa Pwani.

Mwakilishi wa asasi ya miradi ya maendeleo ya jamii kutoka Paris nchini Ufaransa, Giacomo Spigarelli alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita huku akisisitiza kuwa ni ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha anakabiliana na tatizo hilo kutokana na mradi huo kwenda sambamba na ujenzi wa viwanda.

“Ujenzi wa bandari unaweza kusababisha athari za mabadiliko ya tabianchi na kijamii, kwa sababu katika mradi huo kutakuwa na viwanda vikubwa zaidi ya 1,000 vitakavyojengwa.

“Vilevile bandari itakuwa na meli nyingi zinazoweza kusaba-



“Shughuli za kibashara (Bagamoyo) zitasababisha uchafuzi wa mazingira kutokana na msongamano wa watu, hivyo ni vema tuanze kupenda kufanya usafi wa mazingira yetu kuanzia sasa.”

Mwakilishi wa asasi ya miradi ya maendeleo ya Jamii kutoka Ufaransa, Giacomo Spigarelli.

bisha uchafuzi wa mazingira na hewa kutokana na matumizi ya mafuta,” alisema Spigarelli.

Mratibu wa miradi ya asasi hiyo nchini, Magesa Nathanael alisema wanaunga mkono jitihada za

jumuiya za kimataifa za kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa kujitolea kufanya usafi wa mazingira.

Ofisa mipango wa asasi hiyo Bagamoyo, Betha Mollel alisema hali ya usafi siyo nzuri wilayani hapa kutokana na takataka nyingi kuzagaa katika maeneo mbalimbali.

“Tumejitolea kufanya usafi katika Kata ya Magomeni A kwa kushirikiana na halmashauri lakini hali siyo nzuri majumbani, tumekuta takataka nyingi mno, wananchi wana ari ya kukusanya takataka na kuzihifadhi katika mifuko, lakini gari wanadolitegeme halifiki kuzichukua,” alisema Mollel.

Mwenyekiti wa Seikali ya Mtaa wa Magomeni A, Mwinyi Vuguvugu alisema gari la kuzoa takataka halifiki eneo hilo licha ya wananchi kuwa na utayari wa kuzikusanya na kuhifadhi.

“Takataka hukaa muda mrefu bila ya kwenda kutupwa katika dampo lililotengwa na halmashauri,” alisema Mwinyi.